

BUKU LA 12**9/25/2020**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Katika msimu huu wa mafunzo ya mtandaoni na kupanga kufungua shule, mara nyingi tunasikia "Tuko pamoja," na ninaendelea kuona ni kweli hapa DCSD. Ni muhimu kufanya kazi na washirika wetu wa jamii katika kufanikisha kazi kubwa ambayo tunafanya kila siku. Timu yetu ya uongozi wa DCSD inaendelea kujishughulikia na kupokea maoni kutoka kwa washika dau wetu wakiwa lengo la kuboresha mawasiliano katika jamii yetu yote.

Mfano mzuri wa ushirikiano wa washika dau wa jamii wanaotumika ni Baraza la Ushauri la Wakuu (PAC). PAC inaundwa na wazazi, wafanyakazi wa shule, wanafunzi, na wanajamii. Juhudi zao zinatunga mkono kwa kushirikiana na kutoa maoni ya kuongeza mafanikio na utendaji wa mwanafunzi ikiwa ni pamoja na:

1. Kudumisha mtazamo wa shule nzima kuhusu maswala.
2. Katenda kama kiungo kati ya shule na jamii.
3. Kuhamasisha ushiriki wa wazazi na washika dau wengine ndani ya jamii ya shule.
4. Kushughulikia kuongeza mafanikio na utendaji wa mwanafunzi kupitia shughuli za uwazi na mazoea bora ya pamoja.

Hongera kwa wanachama wetu wapya waliochaguliwa wa PAC! Tafadhali angalia [tovuti ya PAC](#) kupata taarifa za sasa na maelezo ya uchaguzi kurudiwa.

Wiki ijayo, tutafanya mkutano wa kikundi cha kuangazia cha Baraza la Ushauri la Mkuu wetu. Walimu, wanafunzi, na vikundi vyetu vya ushauri wa familia pia wataandaa majadiliano katika siku za usoni. Ningependa pia kushukuru viongozi wetu wa jamii ya wafanyabiashara ambao ni Baraza letu la Ushauri la Msimamizi (SCAC). Baraza hizi na ushirikiano wao hutoa mchango wa thamani ambao ni muhimu kufikia malengo ya wilaya yetu. Ninashukuru sana watu wengi ambao wanashiriki na wao kutaka kuhudumia jamii yetu.

Kufungua Shule Tena Ana kwa Ana

Jopo Kazi la Kufungua Tena la DCSD COVID-19 litaendelea kukaribisha vikundi vya kuangazia ili kuelewa vizuri mahitaji na wasiwasi wa familia zetu za DCSD na pia waalimu na wafanyakazi wetu. Maoni yaliyokusanywa kutoka kwa vikundi hivi vya kuangazia yatatusaidia kuboresha mpango wetu wa kurudi tena. Nashukuru wengi wenu ambao mmechukua muda kutoka kwa shughuli zenu ili kushiriki katika mazungumzo haya. Chati hapa chini inaelezea shule za DCSD kufunguliwa tena. Tena, tutawarudisha tu wanafunzi kwa mafunzo ya ana kwa ana wakati hatari ya COVID-19 kuenea inakuwa wastani au inapungua - chini ya visa 100 kwa watu 100,000 katika kipindi cha siku 14.

Data ya Mitindo ya Sasa ya COVID-19

Kama kikumbusho, Jopo Kazi la Kufungua Tena la DCSD COVID-19 hukagua tovuti ya GDPH kila siku baada ya saa 3:00 ili kufuatilia data ya mitindo ya sasa ya Jimbo la DeKalb na Georgia.

Tafadhali tembelea <https://dph.georgia.gov/covid-19-daily-status-report> baada ya 3:00 kila siku ili uone maelezo ya sasa.

Habari Njema

Ninajivunia walimu wetu na shule nyingi, kama Chuo cha DeKalb cha Mafunzo ya Mapema (DECA), ambacho kimepewa jina tu kama Shule ya Kitaifa ya Blue Ribbon. Hii ni heshima sana. Utambuzi huo unategemea utendaji wa jumla wa kitaaluma wa shule au maendeleo ya kuziba mapungufu ya mafanikio kati ya vikundi ndogo vya wanafunzi. Nampongeza Dk. Michelle Jones, Mkuu wa Chuo Edward Conner, wafanyakazi wa DECA, na muhimu zaidi, wanafunzi wetu kwa kupata mafanikio haya ya kitaaluma. Hakikisha kuangalia [hadithi zetu za tovuti](#) kupata habari njema zaidi!

Nilihudhuria Mkutano wa Lakeside Cluster na ninathamini sana ushirikiano wao. Shukrani za pekee kwa Mwanabodi Bi. Allyson Gevertz (Wilaya ya 4), Msimamizi wa Mkoa II Bw. Trenton Arnold, na wakuu ambao walishirikiana jinsi wanavyowasaidia walimu wetu na wanafunzi wakati huu. Ningependa pia kuwashukuru Kamati yetu ya Ushauri ya Wanafunzi ambao nilikutana nao kupitia mtandao na ninatarajia kuona kazi ya kipekee ya wanafunzi wetu!

Ninataka kukumbusha kila mtu katika jamii yetu kuendelea kuwa hodari wakati huu wa dhiki, haswa kwani tunaweza kuona mzozo wa umma na dhuluma za kijamii zikitendeka karibu nasi. Tafadhali fahamu kwamba washauri, wafanyakazi, na waalimu wa DCSD wanapatikana kila wakati kusaidia kuongoza wanafunzi na familia zao kupitia majadiliano magumu lakini muhimu kuhusu rangi, utofauti, na ujumuishaji.

Kama marehemu John Lewis alishiriki, “Hakuna kitu kinachoweza kuzuia nguvu ya watu waliojitolea na walioamua kufanya mabadiliko katika jamii yetu.” Ninaamini kwa moyo wote kuwa pamoja tunaweza kutoa zana na rasilimali kwa wanafunzi wetu wachanga kuleta mabadiliko katika ulimwengu sasa na katika siku zijazo. Asante kwa kufanya kijiji hiki kiwe thabiti, kutoa maoni yako, na kusaidia wanafunzi wetu wanapofanikiwa kupitia mtandao.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris